

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Mtaa wa Sheikhbad,  
S.L.P. 1004,  
65101LINDI,  
Barua Pepe: [rbclindi@pccb.go.tz](mailto:rbclindi@pccb.go.tz).

**TANZANIA.**  
[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

**LINDI**  
**17 Machi, 2021**

## **TAARIFA KWA UMMA**

### **TAKUKURU MKOA WA LINDI YAWAFIKISHA MAHAKAMANI WATUHUMIWA WAWILI KWA TUHUMA ZA KUTOA NA KUPOKEA RUSHWA SH. 50,000/= WILAYANI LIWALE**

**Ndugu wanahabari,**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Lindi inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya kuzuia na kupambana na rushwa ili kuimarisha utawala bora na kuhakikisha haki inatamalaki.

**Ndugu wanahabari,**

Leo tumewaita tena ili muweze kuuhabarisha umma kuwa Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Lindi, leo tumewafikisha mahakamani watuhumiwa wawili (2) ambao uchunguzi wa tuhuma dhidi yao umekamilika.

Watuhumiwa hao ni:

1. Abdu Abdala Licho, Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mahonga wilaya ya Liwale.
2. Alberto Joseph Mwambani, Dereva mkazi wa wilaya ya Ruangwa

**Ndugu wanahabari,**

Mnamo tarehe 9 Februari, 2021 TAKUKURU Wilaya ya Liwale ilipokea taarifa kutoka katika vyanzo vyetu vya siri, ikielezea kwamba Afisa Mtendaji wa Kijiji cha Mahonga Ndugu Abdu Abdala Licho alikuwa ameenda baa inayojulikana kwa jina la “Rena Pub” akiwa na muhuri wa

ofisi ya kijiji hicho ili kusaini nyaraka za mauziano ya shamba. Aidha, chanzo hicho kilieleza kwamba kuna viashiria vya kufanyika vitendo vya rushwa.

**Ndugu wanahabari,**

Kama ilivyo ada baada ya kupokea taarifa hizo, TAKUKURU Wilaya wa Liwale ilifanya uchunguzi mara moja kwa lengo la kubaini na kuthibitisha ukweli wa tuhuma hizo, ambapo ilibainika kuwa Alberto Joseph Mwambani alimpatia Abdu Abdala Licho fedha Sh.50,000/= kama asante baada ya kusaini nyaraka hizo za mauziano na kutumia muhuri wa Mtendaji wa Kijiji cha Mahonga. Vitendo hivi vinaangukia katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2019.

**Ndugu wanahabari,**

Baada ya TAKUKURU Wilaya ya Liwale kukamilisha uchunguzi watuhumiwa hao wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya Liwale na kufunguliwa Kesi ya Rushwa Namba 01/2021 mbele ya Hakimku Mkazi Mfawidhi Mh. Erasto Philly kwa makosa chini ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura ya 329 Marejeo ya Mwaka 2019 kama ifuatavyo:

1. Kutoa asante/ zawadi
2. Kupokea asante

Baada ya kusomewa hati ya mashitaka na Mwendesha Mashitaka wa TAKUKURU Wakili Osborn Paissi, mtuhumiwa Alberto Joseph Mwambani amekiri kosa la kutoa asante na hivyo mahakama kumkuta na hatia na kumuamuru kulipa faini Sh. 600,000/= au kwenda jela miaka miwili. Mtuhumiwa huyo amelipa faini. Kwa mtuhumiwa Abdu Abdala Licho amekana shitaka, hivyo atadhaminiwa hadi kesi itakapokuja tena kwa ajili ya hatua nyingine

**Ndugu wanahabari,**

TAKUKURU mkoa wa Lindi inaendelea kutoa rai kwa watumishi wa umma na wananchi kwa ujumla kujiepusha na vitendo vyovyote vya Rushwa kwani kila mmoja wetu anajua madhara yatokanayo na vitendo vya Rushwa, na kamwe TAKUKURU kwa kutumia mamlaka tuliopewa kwa mujibu wa sheria hatutasita kuendelea kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani wale wote ambao wanajihusisha na vitendo vya Rushwa.

Pia nichukue nafasi hii kutoa rai kwa watumishi wote wa serikali na sekta binafsi katika mkoa wa Lindi kuwa Taifa letu linahitaji maendeleo, hivyo kila mmoja wetu anatakiwa kuendelea kuzingatia viapo vya utumishi na maadili ya kazi zake, pamoja na kufahamu kuwa Rushwa haijawahi kukubalika mahali popote na katika jamii yoyote ile.

**Ndugu wanahabari,**

TAKUKURU Mkoa wa Lindi inaendelea kuwashukuru wananchi, vyombo vya Habari, pamoja na taasisi mbalimbali (binafsi na za serikali) katika Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kuutoa kwa ofisi zetu ikiwepo kutoa taarifa mbalimbali za vitendo vya rushwa. Aidha, tunawaomba wananchi na wadau wote waendeleo kutuunga mkono kwa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa kutumia njia mbalimbali hususani kupitia simu yetu ya bure ya namba ya dharura **113** kwani mapambano dhidi ya rushwa si ya TAKUKURU peke yake bali ni ya jamii nzima kwa ujumla.

**Imetolewa na:**

Eng. Abnery J. Mganga  
**Mkuu wa TAKUKURU (M) Lindi**